TANGAZO LA SERIKALI NA. 384 la tarehe 15/5/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA. 287)

# KANUNI ZA KUDUMU

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 70(1))*

KANUNI ZA KUDUMU (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA SAME, ZA MWAKA 2020

Jina

1. Kanuni za Kudumu hizi zitajulikana kama Kanuni za Kudumu (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Same za Mwaka 2020 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Same za Mwaka 2017 ambazo katika Kanuni hizi zitajulikana kama "Kanuni za Kudumu Kuu".

Tangazo la Serikali Na 114/2017

Marekebisho ya Kanuni ya 2

2. Kanuni ya 2 ya Kanuni za Kudumu Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kuongeza tafsiri ifuatayo:

"kauli zenye kashfa" maana yake ni maneno yenye kejeli, uongo, matusi au yenye kuhusu jambo la aibu ambayo hayapaswi kuzungumzwa kwenye vikao vya Halmashauri au Kamati zake;

Marekebisho ya Kanuni ya 27

3. Kanuni ya 27 ya Kanuni za Kudumu Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta Kanuni Ndogo ya (3) na badala yake kuweka Kanuni Ndogo mpya ifuatayo:

"(3) Mjumbe aliyesimamishwa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2) ya Kanuni hii atapoteza haki zake zote ikiwa ni pamoja na haki ya kulipwa posho na nauli kwa muda wote atakaokuwa

amesimamishwa."

Marekebisho ya kanuni ya 67

4. Kanuni ya 67 ya Kudumu Kuu inafanyiwa marekebisho kwa-

(a) kufanya masharti ya kanuni hiyo kuwa masharti ya kanuni ya 67(1); na

(b) kuongeza kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

"(2) Masharti ya kuvunja Mkataba ni kwa mujibu wa Sheria ya Mikataba Sura ya 345."

Marekebisho ya kanuni ya 75

5. Kanuni ya 75 ya Kanuni za Kudumu Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno "kama nakala zinapatikana" yaliyo katika kanuni ndogo ya (1).

Nyongeza ya kanuni ya 88A

7. Kanuni za Kudumu kuu zinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza Kanuni mpya ya 88A baada ya Kanuni ya 88 kama ifuatavyo:

"88A (1) Mjumbe ambaye hataridhika na uamuzi wa Mwenyekiti alioutoa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu anaweza kukata rufaa kwenye Kamati ya Maadili.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ndogo ya kwanza Mjumbe atawasilisha rufaa kwa maandishi kwa Katibu wa Kamati ndani ya masaa arobaini na nane tangu kutolewa kwa uamuzi unaokatiwa rufaa.

(3) Mjumbe anayekata rufaa atatakiwa kuwasilisha maelezo ya rufaa yanayoainisha yafuatayo-

(a) jina la mjumbe anayekata rufaa;
(b) jina na cheo cha mlalamikiwa;
(c) tarehe, muda na mahali uamuzi

ulipotolewa;

(d) vielelezo na majina ya mashahidi kama wapo.

(4) Kamati ya Maadili haitashughulikia:-

(a) rufaa iliyochelewa kuwasilishwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

(b) rufaa ambayo haijawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (3).

(5) Kamati ya Maadili itatakikiwa kutoa uamuzi wa rufaa ndani ya muda wa siku thelathini tangu tarehe ya kuwasilishwa kwa rufaa.

(6) Uamuzi wa Kamati ya Maadili utatolewa kwa maandishi na endapo mjumbe aliyekata rufaa hatoridhika na uamuzi wa Kamati hiyo anaweza kukata rufaa kwa Mkuu wa Mkoa ndani ya siku saba tangu tarehe ya kutolewa kwa uamuzi.

(7) Mkuu wa Mkoa atatakiwa kutoa uamuzi wa rufaa ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kuwasilishwa kwa rufaa na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Same umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio la Kikao cha mkutano wa baraza la Halmashauri uliofanyika tarehe 15/3/2018 na kubandikwa mbele ya:-

ANNA CLAIRE SHIJA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

CHRISTOPHER M. IRIRA (DIWANI),
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,Same*

NAKUBALI,

L.S

*Dodoma,*
16 Aprili, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN OR-TAMISEMI*
*Dodoma*